**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU**

**SHULE YA SEKONDARI BISHOP NICODEMUS HHANDO**

MKUU WA SHULE: **0627758722**

MAKAMU MKUU WA SHULE: 0625977328

S. L. P 258, MBULU, MANYARA-TANZANIA TAREHE: …………..

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ________________________________________**

**S.L.P ___________________________________________**

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BISHOP NICODEMUS HHANDO, HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU, MKOA WA MANYARA, MWAKA …………….**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule hii mwaka ……… na atasoma tahasusi ya ………… **HONGERA** sana kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii

Shule ya Sekondari BISHOP NICODEMUS HHANDO ipo umbali wa **Kilometa 17** kutoka makao makuu ya **Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.** Shule ipo kando ya barabara kuu kutoka Arusha kwenda Haydom kupitia Mbulu. Usafiri wa basi kutoka mjini **MBULU** unapatikana katika kituo cha mabasi Mbulu Nauli ni Shilingi 4,000, unashuka kwenye geti la shule. Ukitokea Dongobesh au Haydom utashuka pia kwenye geti la shule

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe …………** Mwisho wa kuripoti ni **tarehe ……………….** Jitahidi kuwahi ili usipoteze nafasi hii adhimu uliyopewa na serikali

1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

**SARE ZA SHULE**

- **i.** suruali rangi kahawia pea mbili. Utajishonea-juu rinda mbili mbele, chini mkunjo wa juu(turn up).
- **ii.** shati nyeupe(Halwa) mikono mirefu pea mbili utajishonea/kujinunulia
- **iii.** Tai ndefu nyeusi yenye mchirizi mweupe.
- **iv.** soksi nyeusi jozi mbili.
- **v.** sweta moja-rangi kahawia shingo V
- **vi.** Aje na T-shirt ya shule yenye nembo, rangi ya njano colar form six au atanunulia shuleni kwa shilingi 15,000/=
- **vii.** Sare za michezo:- Track suti rangi ya njano, tisheti 1 ya kijani isiyo na maandishi yoyote, shingo duara na raba nyeusi pea mbili
- **viii.** Viatu vyeusi vya shule pea mbili vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
- **ix.** Suruali 1 ya kazi rangi ya kaki mshono rinda kwa ajili ya kazi za nje na maandalizi ya masomo ya usiku na pullneck (kabakoo) nyeupe
- **x.** Mkanda mweusi uwe wa ngozi

2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

**i.** Madaftari 10 (counter book Q4), kalamu za kutosha, **Ream Mbili (A4)** aina ya **"paper Aone" au" Paperline"** kwa mwaka

**ii.** Mwanafunzi kwa TAHASUSI yake anashauriwa kujinunulia vitabu vya ziada na kiada. (Atashauriwa na mwalimu wake wa somo hata baada ya kuripoti)

**iii.** Barua ya maagizo (Joining instruction)

**iv.** Vyeti vyako (Vivuli vya vyeti) vya kidato cha nne (IV) Academic, Leaving na cheti cha kuzaliwa.

**v.** Cheti cha daktari (medical Examination Certificate) ambacho kimejazwa vizuri na Mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.

**vi.** Fomu ya makubaliano ya mzazi kumsomesha mwanae (Fomu zimeambatishwa nyuma ya barua hii.

**vii.** Mto mmoja na foronya 2 za rangi ya blue bahari.

**viii.** Mashuka Jozi 2 rangi ya **PINK**, blanket 1 nzito, chandarua 1 ya mstatili rangi ya blue.

**ix.** Taulo (1)

**x.** Mwavuli 1, buti ya matope kwa ajili ya shughuli za nje wakati wa mvua.

**xi.** Aje na Godoro inch 3 kwa futi 2¹/2.

**xii.** Vyombo vya chakula: - Sahani ya bati, (Aluminium) kikombe, bakuli na kijiko.

**xiii.** Sanduku la bati/chuma la kufunga kwa kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyako.

**xiv.** Mwanafunzi aje na **BIMA** ya Afya kwa ajili ya matibabu yake

**xv.** NB: Gharama nyingine ya dawa nje ya bima atagharimia mzazi, shuleni tunatoa huduma ya kwanza tu.

**xvi.** Ndoo moja (1) yenye ujazo wa lita 10 zenye mifuniko kwa matumizi yake binafsi.

**xvii.** Jembe 1 lenye mpini imara kwa ajili ya kazi za shule, FVYHMopa 1, kwanja/fyekeo 1, soft broom 1 na hard broom 1 kwa ajili ya kufanyia usafi.

- **Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 75,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB**: Fedha zilipwe Benki kwa **Ac.No. 41201000018** Bank ya **NMB**. Jina la Ac. **BISHOP NICODEMUS HHANDO SEKONDARI.**

Utakapofika shuleni unatakiwa kuwasilisha **"bank pay-in slip"** kwa mhasibu wa shule ili akuandike kwenye daftari maalum.

Kila mwanafunzi atagharamia mahafali mwaka kwa mwaka na uchapishaji wa cheti (ADVANCED LEAVING CERTIFICATE) mwaka wa mwisho wa masomo yake .

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

1. **Sheria na Kanuni za Shule**
   - i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
   - ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
   - iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
   - iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
   - v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
   - vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
   - vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
   - viii. viii.Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
   - ix. Kutunza mali za shule;
   - x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
   - xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
   - xii. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

***MUHIMU:***

- ***Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;***
- ***Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.***
- ***Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa tu).***

2. **Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**
   - i. Wizi;
   - ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
   - iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
   - iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya kimapenzi, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; n.k.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kukutwa na simu au kifaa chochote cha muziki/umeme
xix. Kutoka nje ya shule bila kibali maalum toka kwa uongozi wa shule

- **Viambatisho na Fomu Muhimu**
  i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
  ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
  iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB*: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.***

***TAFADHALI* UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA**

**SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **0627 758 722 Mkuu wa shule**
- **0625 977 328 Makamu mkuu**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

__________________________

ARSENI L. PANGA

MKUU WA SHULE

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM) AMBAYO ITAJAZWA NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Wilaya) ______________________________

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)

______________________________________________

Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:-

**(a) HALI YA MWILI: -**

i. Mapigo ya moyo ______________________________
ii. Haemoglobin (HB) ______________________________
iii. Kundi la damu (blood group) …………………………………………
iv. Mkojo (Urine) ……………………………………………………..
v. Kinyesi (stool) ……………………………………………………..
vi. Macho (Eye) ………………………………………………………
vii. Masikio (Ear)………………………………………………………
viii. Angalia: - Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i) – (vii)

**(b) MAGONJWA**: -

*Amewahi/hajawahi/ana/hana/magonjwa yafuatayo:-

(a) Pumu……………………………………………………………………

(b) Kifua kikuu…………………………………………………………..

(c) Kifafa……………………………………………………………………

(d) Shinikizo la damu chini/juu…………………………………………......

(e) Vidonda vya tumbo..…………………………………………………………

(f) Maradhi ya zinaa………………………………………………………......

(g) Ukoma……………………………………………………………………

(h) Mental illness (ugonjwa wa akili )

……………………………………………………………………………..

(i) Maradhi mengine yasiyotajwa hapo juu:-

………………………………………………………………………………

**SAHIHI NA MHURI WA DAKTARI /MGANGA**

**TAREHE …**…………………………

**FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE**

**SEHEMU A (Ijazwe na mwanafunzi)**

1. Jina la mwanafunzi (majina matatu) ……………………………………….

2. Uraia………………………………………………………… ……………………

3. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………

4. Shule anayotoka ……………………………………………….................

5. Tarehe ya kutoka shule hiyo ………………………………………………...

**SEHEMU B. (Ijazwe na mzazi / mlezi)**

1. Jina la mzazi / mlezi (majina matatu) ……………………………………….

2. Anwani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………

3. Mahali anapoishi ……………………………………………………………..

4.Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi(namba ya simu)…………………………………

5. Kazi ya mzazi/ mlezi …………………………………………………………

Mahali anapofanya kazi ……………………………………………………..

6. Ndugu wawili wa karibu (wanaweza kuwa badala ya mzazi)

***NB:Mwanafunzi atatembelewa Jumapili ya mwisho wa mwezi tu***

Jina la Ndugu wa I…………………………………..…Namba ya Simu…………
Anuani yake: ……………………………………….…Uhusiano……………… Jina la Ndugu wa II: ……………….…………….Namba ya Simu……………… Anuani yake …………………………….…Uhusiano wake : ……………………
TAREHE:…………………… SAHIHI YA MZAZI:………………………

13

**FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUMSOMESHA MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………… wa kijiji cha/mtaa
wa …………………… …. Kata ya ………………………………Halmashauri
ya…………………………… Ambaye ni mzazi/mlezi
wa ……………………………………...……………..

Anayeingia kidato cha **TANO** katika shule ya sekondari

Bishop Nicodemus Hhando najifungia wajibu huu kwa ajili ya kumsomesha mwanafunzi tajwa hapo juu mbele ya utawala wa kijiji changu hiki. Nimesoma barua ya kumwita shuleni, sheria za shule na fomu zote zilizoambatishwa, nimeelewa kila kitu na kuridhika. Pia najua nisipotimiza masharti yote mwanafunzi huyu hatopokelewa shuleni. Nakubali ahadi hiyo nikijua ni ahadi ambayo sitaweza kuikiuka bila hatua za kisheria zinazostahili kuchukuliwa dhidi yangu.

Sahihi ya mzazi au mlezi …………………………….. Tarehe ……………….. sahihi ya afisa mtendaji kijiji/Mtaa …………….Tarehe …………Namba ya simu……….